UTARATIBU WA GLOBAL FUND KATIKA UTOAJI WA FEDHA NA MCHAKATO WA USHIRIKI WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI

KWA AJILI YA ASASI ZA KIRAIA

JUNI 2009

YALIYOMO

Orodha ya vifupisho ……..… 2

1.0 Utangulizi ……..…….. 3

1.1 Lengo la Kitabu hiki ni nini? …… 3

1.2 Kitabu kinawahusu kina nani? ……. 3

2.0 Kuhusu Global Fund ……..….. 4

2.1 Global Fund Ni Nini? ……..…… 4

2.2 Global Fund Ilianzaje na Lini? ……..…… 4

2.3 Misingi ya Utendaji wa Global Fund ……..……... 5

2.4 Utaratibu wa Global Fund Katika Michanganuo ……. 5

2.5 Utaratibu wa Utoaji Fedha wa Global Fund …..……... 9

3.0 Tanzaia na Global Fund ……..… 10

3.1 Tanzania National Coordinating Mechanism (TNCM) …. 10

3.2 Katika Ngazi ya Tanzania Utekelezaji Ukoje ……..... 11

3.3 Matatizo ya Utekelezaji ……..... 11

3.4 Nini Cha Kufanya? ……..……. 12

4.0 Kiambatanisho, Anwani za wawakilishi wa AZAKI ……... 14

Orodha ya vifupisho vya maneno muhimu

AMREF	Mmoja wa PR anayeshughulika na mashirika yasiyo ya kiserikali.
AZAKI	Asasi za kiraia.
CBO	Mashirika madogo ya kijamii.
G8	Nchi 8 Tajiri duniani. Nchi hizo ni Canada, Italia, Ufaransa, Ujerumani, Japan, Urusi, Uingreza na Marekani.
GFATM	Mfuko wa fedha wa Dunia wa kupambana na UKIMWI, kifua kikuu na Malaria.
LFA	Kampuni moja inayochaguliwa kila nchi itakayo kuwa mhakiki wa Global Fund na kutoa taarifa juu ya matumizi ya fedha za Global Fund.
LSR	Shirika lililo chini ya PR ambalo linapokea fedha kutekeleza mradi na kupeleka nyingine kwa SSR.
PR	Shirika linalopokea fedha kutoka Global Fund kwa lengo la kutekeleza program tarajiwa au kugawia wengine watakao tekeleza miradi.
PSI	Mmoja wa PR anayejishughulisha na ugawaji wa Kondom.
SR	Mdau aliyekubaliwa na PR kupokea fedha ili kutekeleza Mradi fulani.
SSR	Huyu ni mdau aliyekubaliwa na SR kupokea fedha ili kutekeleza Mradi.
TAF	Shirika mwavuli kwa mashirika yasiyo ya Kiserikali yanayojihusisha na UKIMWI, Sera na Jinsia nchini Tanzania.
TNCM	Chombo kikuu cha kitaifa kinachosimamia utekelezaji wa Shughuli za Global Fund nchini. Kinaundwa na wadau mbalimbali.
TRP	Kamati ya kiufundi iliyopo Geneva ya kupitia michanganuo na kutoa mapendekezo kwa Global Fund ili itoe fedha au la.
VVU	Virusi vya UKIMWI

1.0 UTANGULIZI

1.1 Lengo la Kitabu hiki ni nini?

Lengo la Kitabu hiki ni kutoa mwanga kwa mashirika yasiyo ya kiserikali/ Asasi za kiraia juu ya Global Fund na taratibu zake mbalimbali tangu kutangazwa kwa wito wa mchanganuo hadi utoaji wa fedha. Kitabu hiki pia kinaeleza namna ambavyo mdau anayejishughulisha na UKIMWI, Kifua Kikuu au Malaria anavyoweza kushiriki katika mchakato huu na nani wa kuwasiliana naye endapo anataka wazo lake lifikie chombo cha juu cha kufanya maamuzi nchini juu ya Global fund kiitwacho kwa kifupi TNCM.

TAF imehudhuria mkutano wa Kikanda mjini Kampala juu ya Global Fund, hivi karibuni na kugundua kuwa yako mashirika machache yanayoshiriki katika miradi ya Global Fund hapa Tanzania. Hivyo umeonekana umuhimu wa kuandika Kitabu hiki kinachoeleza utaratibu mzima wa Global Fund, ili kuongeza uelewaa wa wadau na hatimaye kuongeza idadi ya mashirika yanayoshiriki katika Miradi ya Global Fund.

Ni matumaini ya TAF kuwa utafaidika na taarifa zilizomo katika Kitabu hiki na kitakuwa cha manufaa kwako. Endapo utakuwa na maoni, maswali au taarifa nyingine za kuboresha kitabu hiki usisite kuwasiliana nasi kwa kupitia barua pepe hii. info@tzaidsforum.org au anwani yetu iliyopo mwisho wa kitabu hiki.

1.2 Kitabu Kinawahusu kina nani?

Kitabu hiki kinawahusu wadau wote, kuanzia vikundi vya kijamii, Mashirika yasiyo ya kiserikali na sekta binafsi yanayojishughulisha na magonjwa kama UKIMWI, Malaria na Kifua kikuu.

2.0 KUHUSU GLOBAL FUND

2.1 Global Fund ni nini?

Global Fund to Fight AIDS, Tuberculosis and Malaria (GFATM), kwa Kiswahili ni Mfuko wa Fedha wa Dunia wa kupambana na UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria. Mfuko huu una makao makuu yake Mjini Geneva nchini Uswisi. Mfuko huu ulianzishwa mwaka 2002 ikiwa ni juhudi za kutafuta fedha na kuzitoa ili kushughulikia program zinazopunguza madhara ya VVU/UKIMWI, kifua kikuu na Malaria katika nchi maskini na zile zenye kipato cha kati. GFATM imeundwa kuimarisha ubia kati ya nchi zinazoendelea, zilizoendelea, sekta binafsi, Asasi za kiraia na jamii zilizoathirika.

Muundo wa GFATM ni kutoa fedha kwa nchi kupitia mchanganuo mmoja uliowasilishwa na nchi ambao unaendana na mipango ya nchi husika. Mpaka sasa GFATM ni chanzo cha fedha zinazotumika kupambana na UKIMWI duniani kwa 20% na 66% kwa kifua kikuu na malaria. Tangu kuanzishwa kwa Global Fund mwaka 2002, imeweza kutoa US$ 15.6 billioni kwa program 572 katika nchi 140 duniani. Taarifa zaidi kuhusu GFATM zipo katika tovuti yake hii: www.theglobalfund.org

2.2 Global Fund ilianzaje na lini?

Majadiliano ya kuanzishwa kwa GFATM yalifanyika miaka ya 2000 na 2001. Wakuu wa nchi 8 tajiri duniani (G8) katika mkutano wake mjini Okinawa, Japan uliofanyika mwaka 2000 walitoa wito wa kuundwa kwa Mfuko huo (GFATM). Katika kikao cha maraisi wa Afrika kilichofanyika mwaka 2001 mjini Abuja, Nigeria, walitoa wito wa kuanzishwa mfuko huo na wito mwingine ulitolewa na katibu mkuu wa Umoja wa mataifa wa wakati huo Kofi Annan (kwa sasa amestaafu). Mkutano mkuu wa Umoja wa mataifa; kikao maalum kuhusu UKIMWI cha mwezi Juni 2001 kilitoa agizo la kuundwa mfuko huo. Mwezi julai 2001, nchi hizo 8 tajiri duniani, zilikutana mjini Genoa, Italia na kuchanga fedha kwa ajili ya uanzishaji wa mfuko huo. Kamati maalum iliundwa ambayo ilitengeneza muundo wake na ikakamilika Januari 2002. Fedha ya kwanza kutolewa na GFATM ilikuwa mwezi Machi 2002.

2.3 Misingi ya utendaji wa GFATM

GFATM inafanya kazi kwa kufuata misingi iliyomo katika "katiba" ya kuanzishwa kwake ambayo ni 11, lakini kwa ufupi misingi yake ni kama ifuatayo:-

1. GFATM ni chombo cha kutoa fedha, siyo mtekelezaji. kwa vile Global Fund siyo mtekelezaji, hailazimiki kuwa na ofisi katika nchi zinazotekeleza shughuli za UKIMWI chini ya ufadhili wa Global Fund.
2. Mipango ni ya ki-nchi, inasimamiwa na nchi, ikitengenezwa kwa kushirikisha sekta zote (Serikali, Asasi za kiraia na sekta binafsi).
3. Mfuko unalenga utekelezaji unaojali matokeo zaidi.
4. Mfuko unalenga kujenga na kuimarisha ubia kati ya vyama vya kiraia, sekta binafsi na Serikali na kuzisaidia jamii zilizoathirika na watu wanaoishi na magonjwa haya.

2.4 Utaratibu wa GFATM katika michanganuo

Global Fund imejiwekea utaratibu wa namna michanganuo inayotoka katika nchi inavyopaswa kuandaliwa na namna ya kuiwasilisha. Kielelezo na. 1 kinaonesha utaratibu wa Global Fund katika kuitisha michaanganuo hadi kutoa fedha.



Kielelezo na. 1 Utaratibu wa Global Fund kuitisha michanganuo hadi kutoa fedha.

Kwa kawaida Bodi inafanya maamuzi kuwa nchi zilete michanganuo. Sekretarieti inatangaza wito wa mchanganuo kutoka katika nchi mbalimbali. Kufuatana na maamuzi ya awali ilikuwa kuwe na wito wa mchanganuo mara moja kila mwaka (mara nyingi mwezi March) na mwisho wa kupokea michanganuo ni miezi minne au mitano baada ya sekretarieti kutoa Tangazo. Lakini kwa mwaka 2008, GFATM ilitoa wito mara mbili kwa mwaka.

TNCM inaandaa mchanganuo kwa niaba ya nchi kwa kuzingatia mahitaji ya Tanzania. Kwa mujibu wa Utaratibu, TNCM inachagua *Principle Recipient (PR)* mmoja au zaidi. PR ni shirika ambalo litapokea fedha kutoka Global Fund kwa lengo la kutekeleza program tarajiwa au kuwagawia wengine SR au SSR watakao tekeleza miradi au program zinazolenga kushughulikia magonjwa hayo matatu. Mara nyingi wadau wa maendeleo wanasaidia nchi katika maandalizi ya mchanganuo.

Mpaka sasa Tanzania ina PR wafuatao:-

1. Wizara ya Fedha
2. Pact
3. PSI
4. AMREF

Hata hivyo Tanzania haijafuata uwazi katika upatikanaji wa hawa PR kwa hiyo bado kuna haja kwa Tanzania kuweka uwazi katika upatikanaji wa PR na ikiwezekana mashirika yasiyo ya kiserikali ya hapahapa yawezeshwe kuwa PR.

Baada ya Michanganuo kukamilika, nchi inawasilisha Geneva kupitia kwa LFA. Mchanganuo yote huwasilishwa kwenye sekretarieti, sekretarieti inaipitia kuona kama matakwa yote yamezingatiwa. Michanganuo yote inayokuwa imetimiza matakwa yote, inapelekwa kwenye TRP *"Technical Review Panel"*. TRP ni kamati ya kiufundi iliyopo Geneva ya kupitia michanganuo na kutoa mapendekezo kwa Global Fund. TRP inatoa pendekezo moja kati ya haya manne kwenye Bodi ya Global fund ili itoe maamuzi:-

1. Toa fedha
2. Toa fedha endapo matakwa fulani yatatekelezwa

3. Wafanye marekebisho na kuwasilisha mchanganuo upya
4. Usitoe fedha

Utoaji wa fedha wa Global Fund unategemea mapendekezo ya TRP na uwepo wa fedha katika mfuko. Sekretatrieti inachagua kampuni moja katika kila nchi itakayo kuwa msimamizi na mhakiki wa Global Fund kuwa fedha za Global Fund na utawala katika mashirika wadau unakwenda vizuri. Kampuni hiyo inaitwa LFA *"Local Funding Agent"*.

LFA anakwenda kwa PR aliyependekezwa na TNCM kumfanyia ukaguzi kuhusu uwezo wake wa kusimamia fedha, uongozi kwa ujumla, miradi, ufuatiliaji na tathmini kisha anatayarisha taarifa na kuipeleka Global fund na kumpa nakala PR inayoonesha nini wameona na nini wamepandekeza. Kulingana na taarifa ya LFA, inawezekana PR akapewa fedha bila kuhitaji msaada wa kitaalam zaidi, au akahitaji msaada wa kitaalam ili aweze kutekeleza vizuri program chini ya Global Fund. Wadau wa maendeleo wanaweza kushiriki katika kujenga uwezo wa PR ili aweze kutekeleza shughuli zake vizuri. Inawezekana mapungufu yatakayogunduliwa yakawa katika mkataba utakaosainiwa kati ya Global Fund na PR ili ayatekeleze kabla ya kuanza kupokea fedha kutoka Global Fund.

Sekretatrieti ya Global Fund na PR wanafanya majadiliano kabla ya kusaini mkataba wa fedha ili kuchambua matokeo tarajiwa na namna ya kuyapima na kutengeneza viashiria. Sekretariate inataarifu World Bank kutoa fedha kwa PR, na PR anatoa fedha kwa SR ili atekeleze mradi kama ilivyoandikwa katika mchanganuo. SR *"Sub Recipient"* ni shirika lililoomba kutekeleza mradi wa Global Fund.

PR anatuma maombi ya fedha nyingine kulingana na taarifa za utekelezaji kila baada ya miezi mitatu (taarifa za maelezo na matumizi ya fedha) anazoandika na kupeleka GFATM baada ya kuthibitishwa na LFA. Kuchelewa kwa ripoti au matumizi mabaya ni mwanzo wa kukosa fedha kwa PR na nchi kwa ujumla.

PR anawasilisha kwa Sekretarieti taarifa ya mwaka ikiwa pamoja na mpango wa kukaguliwa kwa matumizi yake ya fedha (yeye kama PR na SR wake) kupitia kwa LFA. Kigezo muhimu cha kuendelea kupokea fedha za Global Fund ni utoaji taarifa zinazoendana na makubaliano katika mkataba wa fedha ambazo lazima zioneshe matokeo gani yamefikiwa.

2.5 Utaratibu wa utoaji fedha wa GLOBAL FUND

Kielelezo na. 2 kinaonesha baada ya Global Fund kupitisha maamuzi ya utoaji wa fedha.



Kielelezo na. 2: utoaji wa fedha wa Global Fund

3.0 TANZANIA NA GLOBAL FUND

3.1 Tanzania National Coordinating Mechanism (TNCM)

Global fund ilizitaka kila nchi kuunda chombo kitakachosimamia miradi inayotekelezwa na Global fund katika nchi husika. Global Fund walipendekeza chombo hicho kiitwe Country Coordinating Mechanism (CCM) lakini kwa vile hapa Tanzania, CCM inamaanisha Chama Cha Mapinduzi, iliamuliwa chombo hicho kiitwe TNCM.

TNCM ina kutana mara kwa mara ili kupata taarifa za maendeleo ya utekelezaji wa shughuli zinazofadhiliwa na Globa Fund nchini. Hata hivyo, mikutano hii haiongelei kuhusu magonjwa hayo matatu yaani UKIMWI, Kifua kikuu na Malaria bali na magonjwa mengine yatakayojitokeza nchini Tanzania kama mafua ya ndege.

TNCM inawajumbe kutoka katika sekta zote ili kuwa na uwiano sawia. Mwenyekiti wake ni Katibu Mkuu katika ofisi ya waziri Mkuu. Wajumbe wa TNCM katika kamati kuu ni 17 kwa mchanganuo unaooneshwa katika jedwali na. 1 hapo chini:-

Wawakilishi toka Serikalini	Wadau wa Maendeleo	Asasi za kiraia	Sekta Binafsi
Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Ofisi ya waziri Mkuu	Mwenyekiti wa wadau (kitengo cha VVU/UKIMWI)	Waviu wawili (ke na me)	Muungano wa vyama vya wafanyakazi
Wizara ya Afya	Mwakilishi wa Umoja wa Mataifa	Mashirika yasiyo ya Kiserikali	AIDS Business Coaliation Tanzania (ABCT); sekta binafsi
Wizara ya Fedha		Mashirika ya kidini wawili (mwislam na mkristo)	
Tawala za mikoa na Serikali za mitaa	Mwakilishi wa wadau wengine	Chuo kikuu cha Dar es Salaam	Chama cha wamiliki wa vyombo vya habari Tanzania (MOAT)
Jumla = 4	**Jumla = 3**	**Jumla = 7**	**Jumla = 3**

Jedwali namba 1: mchanganuo wa wajumbe katika TNCM.

3.2 Katika ngazi ya Tanzania utekelezaji ukoje?

Baada ya Global Fund kutangaza wito wa michanganuo, Tanzania inafanya yafuatayo:-

- TNCM inakaa na kuunda kamati ndogo kuchambua mianya inayotokana na upungufu wa fedha ambayo inapaswa kuzibwa.
- Kamati hiyo ndogo inafanya uchambuzi na kuwasilisha taarifa yake ndani ya TNCM
- TNCM inaipitia taarifa na kutoa mapendekezo kwa kamati. Ikiwa kuna mapenmdekezo mengi, kamati inaenda kuyafanyia kazi na kuwasilisha tena. Kama hakuna marekebisho zaidi, TNCM inapitisha kama mwelekeo wa kuandikwa kwa mchanganuo wa kitaifa.
- TNCM inatangaza katika gazeti kwa wadau mbalimbali kueleza ni maeneo gani wangependa kushiriki katika utekelezaji endapo fedha itapatikana. Kwa kawaida unatolewa muda wa wadau kuandika na kuwasilisha mawazo hayo. Wadau wanapaswa kuonyesha kama wangependelea kuwa PR, LSR au SR au SSR.
- TNCM inawachagua waandishi wa Mchanganuo kisha kuupitisha katika kikao cha TNCM na kuutuma kwa LFA ili waupitie na kutoa maoni kabla ya kuupeleka Global Fund.

3.3 Matatizo ya utekelezaji wa sasa

Badala ya kufuata utaratibu huo hapo juu, ingefaa kufanya yafuatayo:-

- Wadau washirikiswe kwanza kwa kupewa taarifa kuwa wawasilishe mianya wanayoona wanaweza kuziba kwa kutumia rasilimali za Global Fund katika Round iliyotangazwa. Hii itasaidiaa mianya inayotafutwa itokane na jamii badala ya ofisini.
- Kamati iundwe na TNCM kuweza kupitia mianya iliyowasilishwa na wadau ili iwekwe katika makundi “clusters” na kutoa mwelekeo wa mchanganuo wa kitaifa
- TNCM itenganishe tangazo la kuitisha maelezo ya wadau na kuchaguliwa kwa PR. Hii ni kwa sababu utaratibu uliopo

kwa sasa na vigezo havieleweki sawasawa kwa wadau. Hivyo kutenganishwa kwake kutaongeza uwazi wa namna PR anavyopatikana. Ikiwezekana mashirika ya hapa nchini yawezeshwe kuwa PR badala ya kutegemea mashirika toka nje ya nchi ambayo gharama zao za uendeshaji zipo juu zaidi.

- Mitandao ya mashirika mbalimbali iliyopo, ijenge uwezo wa wanachama wake ili kuweza kupokea fedha za Global Fund na kuzitumia vizuri kwa malengo yaliyokusudiwa.

3.4 Nini cha kufanya ili kushiriki katika miradi ya Global Fund?

- Lazima shirika liwe linafanya kazi katika maeneo ya UKIMWI, Malaria au Kifua kikuu.
- Mashirika mitandao, yajenge uwezo wa mashirika madogo madogo ambayo ni wanachama wake katika maeneo ya utawala wa fedha, utawala wa rasilimali watu, usimamizi wa mashirika, utawala bora, usimamizi makini wa ofisi ili mashirika yaanze kujizoeza kushiriki katika miradi ya Global Fund.
- Mashirika madogo madogo ya kijamii (CBO) yakiisha jengewa uwezo, yatumie elimu hiyo kwa umakini na kuhakikisha kuwa yanakuwa na utekelezaji wa shughuli zake kwa uadilifu.
- Mashirika yajitahidi kuwa na utawala bora katika mashirika yao na kufanya ukaguzi wa hesabu za mashirika yao ili kuthibitishia umma kuwa wana matumizi bora
- TNCM ibadilishe utaratibu wa kupata mwelekeo wa kuandika mchanganuo kusudi mchanganuo uwe wa kitaifa na shirikishi.
- TNCM iweke wazi utaratibu wa kupata PR ili kuweka uwazi wa upatikanaji wao. Mashirika ya kitanzania ambayo yamethibitika kuwa na uwezo yanaweza kuwekewa mkakati wa kufanywa PR ili kuwa na mashirika ya hapa hapa yanayo tekeleza miradi ya hapa nchini.
- Wakati TNCM inapotoa matangazo ya kuitisha maeneo ya kufanyia kazi ili kutoa mwelekeo wa mchanganuo, mashirika yachangamke na kuwasilisha maeneo hayo ili yaweze kuwekwa katika mchanganuo wa kitaifa.
- TNCM iunde kamati ya kufanya uchambuzi wa maeneo yaliyopendekezwa na watekelezaji wa shughuli za kijamii na

kuandaa makundi "clusters" ili kuongeza uwazi. Kamati hii isihusishe PR waliopo ili kupunguza msuguano wa kimaslahi *"conflict of interest"*

- TNCM iwe inatangazia wataalam kutoka katika mashirika ya kitanzania wanaopenda kushiriki katika uandishi wa mchanganuo ili kujenga uwezo wa wataalam zaidi wa hapa nchini badala ya kutumia washauri toka nje ya nchi.

Wasiliana na TNCM kupitia kwa mwakilishi wa kundi husika. Mfano mtu anayeishi na VVU anaweza kuwasiliana na TNCM kupitia kwa mwakilishi wa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI. Jedwali namba 2 linaorodhesha wawakilishi katika TNCM hadi mwaka 2010 kutoka makundi mbalimbali.

S/N	Makundi wakilishwa	Jina	Simu
1	Waviu	1. Mrs. Joan Chamungu 2. Mr. Leonard Lugenge	0755 761905 0754 455 643
2	Mashirika yasiyo ya Kiserikali	1. Dr. Peter Bujari 2. Dr. Samwel Mtulu	0774 217127 0783 505522
3	Mashirika ya kidini	1. Adelina Kimambo 2. Mr. Suleiman Lolila	022 2123730 0754 289100
4	Sekta Binafsi	1. Richard Kasesela	022 2125113

Jedwali namba 2: Wawakilishi katika TNCM hadi mwaka 2010 kutoka makundi mbalimbali

4.0 KIAMBATANISHO Na. 1: MAELEZO YA ZIADA YA WAJUMBE WA TNCM KUTOKA ASASI ZA KIRAIA

Dr. Adeline Kimambo

Anaowawakilisha:	Mashirika ya kidini.
Cheo chake:	Mkurugenzi
Atokako:	Christian Social Services Commission (CSSC), Dar es Salaam
Nafasi katika TNCM:	Makamu Mwenyekiti
Anwani:	P.O. Box 9433, Mtaa wa Ali Hassan Mwinyi.
Simu:	255 22 2123730/2136720
Fax:	255 22 2118552
Barua pepe:	akimambo@cssc.or.tz

Mr Suleiman Lolila

Anaowawakilisha:	Mashirika ya kidini
Cheo chake:	Mratibu, Program ya VVU/UKIMWI
Atokako:	Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA)
Nafasi katika TNCM:	Mjumbe
Anwani:	P.O. Box 21422, Dar es Salaam
Simu:	255 754 289100
Barua pepe:	lolila6@yahoo.com

Dr. Peter Bujari

Anaowawakilisha:	NGO, Mashirika yasiyo ya Kiserikali
Cheo chake:	Mkurugenzi Mtendaji
Atokako:	Human Development Trust (HDT)
Nafasi katika TNCM:	Mjumbe
Anwani:	P O BOX 65147, Mwenge, Barabara ya Coca Cola, Dar es Salaam
Simu:	+255 22 2772264
Fax:	+255 22 2772299
Barua pepe:	ed@hdt.or.tz

Dr Samuel Mtullu

Anaowawakilisha:	NGO, Mashirika yasiyo ya Kiserikali
Cheo chake:	Meneja wa Program
Atokako:	TANGA AIDS WORKING GROUP (TANGA)
Nafasi katika TNCM:	Mjumbe
Anwani:	P.O. Box 1374
Simu:	255 27 2642266
Fax:	255 27 2642266
Barua pepe:	drsamtullu@yahoo.co.uk

Mrs Joan Chamungu

Anaowawakilisha:	Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI
Cheo chake:	Mwenyekiti
Atokako:	Tanzania Network of Women Living with HIV/ AIDS, Dar es Salaam
Nafasi katika TNCM:	Mjumbe
Anwani:	P.O. Box 77704, mtaa wa Amani/Mvita, Kariakoo.
Simu:	255 22 2184595
Barua pepe:	joanchamungu@yahoo.com

Mr Leonard Lugenge

Anaowawakilisha:	Watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI
Cheo chake:	Mwalimu
Atokako:	NACOPHA, Chuo Kikuu cha Ruaha
Nafasi katika TNCM:	Mjumbe
Anwani:	P.O. Box 576
Simu:	255 754 455643
Barua pepe:	leolugenge@yahoo.com

Kimetayarishwa na:
Tanzania AIDS Forum (TAF)
P O BOX 65147,
DAR ES SALAAM
SIMU: +255 22 5509422
FAX: +255 22 2772299
Barua pepe: info@tzaidsforum.org
Tovuti: www.tzaidsforum.org